**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**Tarehe 10 Novemba 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Bushira Yahaya Rashidi
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rioeyongeza
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Omari
Rahma Ali
Sudi Saidi Ramadhan

Wageni :
Venant William
Damas Nderumaki

**Siku ya uamsho wa hali ya majira**
Wageni wawili Venant William (mwana harakati) na Damas Nderumaki (mwana harakati kutoka Tanzania Coalition for Sustainable Development) walikaribishwa na kila mtu walijitambulisha. Damas alitoa mifano ya miradi mengine anayoendesha kama kampeni ya ubora wa mazingira ya Ziwa ya Victoria. Elaine alikutana na Venant kwenye mkutano wa mabadaliko ya hali ya majira kwenye World Social Forum mwezi wa Januari na yeye alitupa contact ya Damas.

Damas na Venant walitoa maelezo kuhusu swala la mabadaliko ya majira kwa wanachama wa UWABA, linasababaishwa na nini na matokea yake. Pia walisema kuendesha baisikeli ni jinsi nzuri kupambana na mabadaliko ya majira kwa sababu haitoi moshi ya carbon kwenye hewa kama magari yanayofanya, na inafaa kwamba UWABA tuandae kwa siku ya uamsho ya mabadaliko ya majira.

Elaine alieleza mpango wa kuendesha baisikeli mpaka Ikulu na Ubalozi wa Merekani kuwapa barua ambazo zitakuwa zimesainiwa na mashirika mbali mbali,, na pia kuwapata waandishi wa habari kuandika kuhusu tukio au kuonyesha tukio. Pia ameandaa barua mbili kwa kiingereza.

Tuliongea kuhusu njia tutafuata na baisikeli na press conference lakini tuliamua kwamba kipau mbele ni kuandaa orodha ya mashirika na kuwaomba wahudhurie mkutano wa wiki ijayo ili tufanye uamuzi huu.

Dominata alitoa mawazo kuhusu vipi kutangaza tukio na alipendekeza tuanze Mnazi Mmoja. Ana contacts wa waandishi wa habari wengi. Mawazo mengine yalikuwa kuwasiliana na radio one, radio Mlimani na JET.

Watu walipendekeza mashirika yafuatayo : Joint Environment Development Action (JEMA), Tanzania Coalition for Sustainable Development (mwenyekiti ni Sylvan Mngaye), Roots and Shoots, University Students Union, EPMS (contact ni Euster), Journalists Environment Tanzania (JET) na Tanzania Assocation of NGOs (TANGO) (Mary Mwingira kiongozi wa TANGO alitupa jina la Samual awakilishe TANGO).

Damas alisema atafuatalia wiki hii ile awe na orodha ya mashirika wataoshirikiana kabla ya jumatano na atakuwa na barua sahihi ambayo mashirika watakubali nayo kabla ya ijumaa. Jumamosi ijayo tunaweza kuandaa mpango zaidi.

Venant alisema atatafsiri barua kwa Kiswahili.

**Msafara wa Baisikeli**

Elaine alimaliza kuandika repoti kwa Ubalozi wa Uholonzi kwa kushirikiana na Mejah, na ijumaa aliwaletea pamoja na photocopy ya risiti, picha na nakala za makala ya gazeti kuhusu msafara. Mbunge Azzan Zungu alimpigia simu Elaine wakati wa wiki kuuliza habari za msafara. Juma alitoa photocopy ya repoti pamoja na picha na makala ya gazeti kwa kumpa Mbunge Azzan Zungu, Kampuni ya Guta, Kampuni ya Bakhresa na Ubalozi wa China (wadhamini wakubwa) na atawaletea wiki ijayo.

DVD ambayo ilitengenezwa na studio ambao walipewa hiyo kazi na Sosthenes inaonyesha siku ya Ibike kututembelea na hotuba kwenye siku ya msafara, siyo msafara yenyewe. Inaonekana kwamba video ya msafara imepotea lakini Sosthenes alimwambia Elaine kwamba bado anafuatalia. Wanachama walikata tamaa kuhusu swala hili. Dominata alisema kulikuwa na mtu mwingine aliyepiga video lakini hakuna mtu amechukua contacts zake.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji**

Elaine alimtembelea Bwana Wemba, mkuu wa idara ya usalama barabarani wa chuo cha usafirishaji wiki hii. Alisema watatoa semina ya bure ya siku moja kwa wanachama wa UWABA kuhusu usalama barabarani chini ya mpango wao wa kuelimisha jamii, na tuandike barua kuomba hudumu hii. Semina itakuwa siku ya jumamosi na tarehe bado hatujaamua. Juma alimletea barua wakati wa wiki na atafuatalia wiki hii. Wanachama walifurahi sana kuhusu mpango huu.

**Ufuataliaji wa barua**
Juma aliwatembelea TANROADS na Halmashauri ya Jiji wiki hii kufuatalia majibu ya barua. Mama Mlamba ambaye yupo Halmashauri wa Jiji alimpa michoro ya mpango wa ujenzi wa Morogoro Road chini ya mradi wa DART. Sehemu zote ya barabara zina sehemu ya baisikeli lakini sehemu nyingine ni embamba na sehemu nyingine zinalindwa kutoka barabara kubwa na miti lakini sehemu nyingine hazilindwi. Lakini wanachama waliona kwa ujumla ni nzuri na wametoa kipau mbele kwa wapanda baisikeli. Alimwambia Juma kwamba tutapata jibu la barua letu kuhusu Dar es Salaam Transport Master Plan.

TANROADS bado hawajajibu barua – Juma anaendelea kufuatalia.

**Ofisi**
Ally Saidi Mohammad alisema kwamba kununua bao laini ya bao za tangazo itakuwa na gharama ya Tsh 50,000. Juma atampa hela hiyo wiki hii (tulichukua Tsh 90,000 kutoka benki kwa ajili ya mipira ya guta lakini mipira ya guta bado hayapatikani).

**Guta**
Spea za Guta bado hazipatikani kwa sababu bado zipo bandarini. Bushira alisema atafuatalia wiki hii.

**Nyinginezo**
Elaine alisema kwamba Violeth ameanza kutafsiri dondoo.

Elaine aliwatumia email kwa Wamba Memorial Fund lakini hajapata jibu bado.

David kutoka Bike Nouveau Italia alisema kwa email kwamba ametutumia mchango (euro 850) lakini bado haijafika akaunti yetu. Elaine atafuatalia wiki hii.